

## Maswali

1. Nani alikuwa mlinzi wa watumishi wa Sulemani?
2. Nani alikutana na Yeroboamu. Alifanya nini?
3. Hii ilikuwa na maana gani?
4. Mbona Mungu alichukua khabila kumi kutoka kwa familia ya Sulemani?
5. Mbona Mungu aliacha mwana wa Sulemani atawale khabila mbili tu?
6. Yeroboamu aliuliza Rehoboamu afanye nini?
7. Wazee walishauri Rehobaomu afanye nini?
8. Rehoboamu alitumia ushauri wa nani?
9. Rehoboamu aliambia watu nini?
10. Yeroboamu alifanya kitu gani kiovu?
11. Watu waliokuwa na imani walienda kuishi wapi?

## Majibu

1. Yeroboamu
2. Nabii Ahiya. Alirarua vazi lake kwa vipande 12. Alimpa Yeroboamu vipande 10.
3. Mungu angempa Yeroboamu khabila 10 kutawala.
4. Kwa sababu Sulemani alikuwa ameacha Mungu.
5. Kwa sababu Mungu alikuwa ameahidi Daudi kwamba mwanawe atatawala juu ya huo ufalme.
6. Fanya maisha ya watu iwe rahisi kwa kupunguza kodi na kazi.
7. Zungumzia watu vizuri, fanya maisha yawe rahisi.
8. Rehoboamu alifuata ushauri wa vijana.
9. Nitafanya maisha yenu kuwa magumu kuliko wakati wa Sulemani.
10. Yeroboamu alitengeneza ndama za dhahabu mbili. Alifanya watu wamwaabudu.
11. Watu waliokuwa na imani walienda Yerusalemku abudu Mungu wa kweli.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM



**Awamu ya 2 Mwaka wa 2**

## 68 Rehoboamu na Yeroboamu

### Kwa Biblia

1 Wafalme 11:26—40 na 1 Wafalme mlango wa 12

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu hutimiza ahadi zake kwa waaminifu. Mungu huadhibu wanaofanya maovu.

### Somo

Sulemani alijenga majengo mengi. Alikuwa na watumishi wengi. Watumishi walisaidia Sulemani na kazi ya ujenzi. Yeroboamu alisimamia watumishi wote kutoka kwa khabila ya Efraimu na Manase. Yeroboamu alikuwa mtu wa maana sana.

Siku moja Yeroboamu alikutana na nabii Ahiya. Ahiya alikuwa amevaa vazi jipya. Ahiya alitoa hilo vazi jipya. Alirarua hilo vazi vipande kumi na viwili. Ahiya alimpa Yeroboamu vipande kumi. Alimwelezea kwamba hivyo vipande kumi ni kama khabila kumi za Israeli. Mungu alisema Yeroboamu atakuwa mfalme. Atatawala khabila kumi za Israeli.

Sulemani alikuwa amegeuka kutoka kwa Mungu. Alioa wanawake wengi wageni. Aliabudu miungu badala ya Mungu. Kwa hivyo baada ya Sulemani kufa Mungu ataondoa khabila kumi kwa familia yake. Mungu alikuwa ameahidi Daudi kwamba wanawe watatala juu ya ufalme wake wakati wote. Mungu atatimiza hiyo ahadi kwa Daudi. Mungu ataacha khabila mbili tu ili mwana wa Sulemani atawale. Lakini atampa Yeroboamu khabila kumi.

Yeroboamu alifurahia sana kwamba yeche atakuwa mfalme. Sulemani alifanya watu kulipa kodi ya pesa nyingi. Aliwafanya wamfanyie kazi ngumu. Walimjengea jumba za wafalme na majengo mengine. Watu hawakufurahia hiyo kodi na kazi ngumu.

Sulemani alikuwa. Rehoboamu alikuwa mwana wa Sulemani. Waisraeli wote walienda Shekemu kumfanya Rehoboamu awe mfalme. Rehoboamu hakuwa mfalme wa nguvu. Aliharibiwa na mali nyingi ya babake Sulemani. Rehoboamu alikuwa mwana wa mke wa asili ya kigeni. Hakuwa amefundishwa njia zote za Mungu. Rehoboamu aliwasanya Waisraeli wote pamoja ili wamtawaze kuwa mfalme.


Watu wote walikuja kumtawaza Rehoboamu kuwa mfalme wa Israeli. Yeroboamu naye alisanya watu wake pamoja. Watu walitaka Rehoboamu akubali kupunguza kodi tena alegeze kazi kabla wamtawaze kama mfalme.

Yeroboamu alizungumzia Rehoboamu kwa niaba ya watu. Yeroboamu aliambia Rehoboamu, "Baba yako alitutoza kodi kubwa. Alitufanyiza kazi ngumu. Ukitulegezea haya yote, sisi tutakutumikia."

Rehoboamu alikubali kuwapa jibu baada ya siku tatu. Kwanza aliuliza wazee wampe ushahuri. Wazee walikuwa wamesikiliza misemo ya Sulemani ya hekima. Walikuwa wazee wenye hekima. Walimwambia, "Kuwa mzuri kwa hawa watu. Fanya kila jambo liwe njema kwao. Halafu watakuanya mfame. Watakuumikia vyema."

Rehoboamu hakuwa na hekima. Hakusikiliza ushauri wa wazee. Rehoboamu alienda kuuliza marafiki zake ushauri. Marafiki walimwambia Rehoboamu aonyeshe watu kwamba yeche ni wa nguvu tena anauwezo kuliko Sulemani. Walimwambia afanye kila kitu ngumu kwa hao watu. Rehoboamu alisikia ushauri mbaya kutoka kwa marafiki zake.

Baada ya siku tatu, Rehoboamu aliambia watu, "Kidole changu kidogo ni kubwa kuliko kiuno cha babangu. Babangu alitaka mlipe pesa nyingi za kodi na kazi ngumu. Nataka mfanye kazi ngumu saidi tena kulipa kodi kubwa saidi. Babangu alimpiga kwa mjeledi. Nitampiga kwa nge." Watu walikasirika sana. Yeroboamu aliwaongoza kinyume na Rehoboamu.



Watu walipiga kelele, "Hatutaki huyu mtu atutawale. Hatuna sehemu kwa ufalme wa Daudi. Hatutawazi Rehoboamu kama mfalme wetu. Tunaenda nyumbani." Rehoboamu aliogopa na kutorokea Yerusalem. Kule alitawala kabilia ya Yuda na ya Benyamin. Ufalme wake uliitwa Ufalme wa Yuda. Rehoboamu alitawala kabilia mbili tu. Mji mkuu wake ulikuwa Yerusalem.

Mungu alimfanya Yeroboamu mfalme wa kabilia zingine kumi. Ufalme wake uliitwa Ufalme wa Israeli. Mji mkuu wake ulikuwa Samaria. Mungu aliahidi Yeroboamu kwamba atambariki ikiwa atawaongoza watu kwa njia ya utauwa. Lakini Yeroboamu alikuwa na tamaa na uchoyo. Hakuwa na haja na ahadi za Mungu.

Ufalme wa Israeli	Ufalme wa Juda
Yeroboamu alitawala kabilia 10	Rehoboamu alitawala kabilia 2
Watu waliabudu mungu wa uongo	Watu waliabudu Mungu wa kweli

Hekalu ya Mungu ilio Yerusalem ndio ilikuwa uti wa ibada. Watu walisafiri kwenda kuabudu Mungu kule. Yeroboamu hakutaka watu wake waende Yerusalem. Wangeamua kumtumikia Rehoboamu tena.

Yeroboamu alitengeneza ndama mbili za dhahabu. Aliambia watu kwamba hao ndama ndio mungu wao. Aliweka ndama mmoja huko Dan kaskazini mwa nchi yake. Aliweka ndama mwingine Bethel kusini mwa nchi yake. Aliweka watu wa kawaida kuwa makuhani na walitoa sadaka kwa mungu wake. Yeroboamu aliwaongoza watu kumuacha Mungu. Alifanya watu waabudu sanamu. Aliongoza watu kufanya maovu makubwa.

Kulikuwa na makuhani wa kweli na Walawi wengi walioishi kwa Ufalme mpya wa Israeli. Walihama na kuenda kuishi Yuda. Walimtumikia Mungu wa kweli. Watu wote waliokuwa na imani kwa Mungu walihama na kwenda Yuda. Waliabudu Mungu kwa Hekalu ya Yerusalem.

Falme hizo mbili, Israeli na Yuda ziliendelea kukaa kwa kutengana. Walikuwa maadui. Yeroboamu alifanya watu wa Israeli kutenda dhambi. Wafalme wa Israeli wote walikuwa waovu. Ufalme wa Yuda ulikuwa na wafalme wengine wazuri. Kulikuwa na watu wachache Yuda waliopenda Mungu.